

## **Utetezi na Kufanya Mabadiliko**

Washiriki watajifunza kuhusu dhana ya utetezi kwa kutambua tatizo linalokumba jamii yao na kutafakari kuhusu mabadiliko mawili wanayotaka kuona siku za usoni kuhusiana na tatizo hilo.

# Je, Utetezi ni nini?

## Sehemu ya Kwanza

### Ambia Wanafunzi Wako

Kuna vigezo vingi vya jumuiya na mazingira yetu tunavyoshukuru kuwa navyo. Pengine tunashukuru kwa kuwa na marafiki zetu. Huenda ikawa kwamba tunafurahia kucheza kwenye timu fulani ya michezo. Pengine tunapenda kuwa na fursa ya kusikiliza muziki mpya kutoka kwa wasanii tunaowapenda.

Hata hivyo, wakati mwingine kuna nyenzo fulani kuhusu jamii yetu ambayo hatupendi. Pengine shule yako imezindua aina mpya ya sare za shule zinazohitaji ununue nguo ghali ilhali huwezi kugharamia. Pengine mwanasiasa anajaribu kutunga sheria ambazo hazitilii maanani mahitaji yetu. Kuna uwezekano kwamba njia za usafiri zilipo mahali tunapoishi hazijaundwa kuweza kutufikisha maeneo ambayo tunahitaji kwenda.

Kwa mfano, uligundua kwamba stesheni za mabasi ziliwalazimisha kuchukua mabasi matatu na kutembea umbali mrefu ndipo muweze kufikia duka kuu lililokaribu.

### Uliza Wanafunzi Wako

Je, unaweza kujaribu kubadilisha hali hiyo?

Je, kuna watu unaoweza kuwasiliana nao ambao wanaweza kukusaidia?

Pengine kuna marafiki zako wanaopitia matatizo sawa na yako. Je, nyote mnawezaje kujitetea?

## Sehemu ya Pili

### Ambia Wanafunzi Wako

Katika hali kama hizi, huwa tunahisi kwamba mambo yangukuwa tofauti ikiwa tunaweza kubadilisha mambo yanayotukera. Hii ari ya kusimama kidete kutetea mambo unayoyaamini na kuleta mabadiliko huitwa “utetezi.”

### Mwingiliano wa Darasa

Kwenye kiwambo kikubwa kwenye sehemu ya mbele ya chumba, kagua tovuti inayotumika kwa ajili ya utetezi. Angazia namna muundo wa utetezi unaonyeshwa humo ulivyoanza kupitia watu, aghalabu vijana ambao waligundua kwamba kuna tatizo linaloathiri jumuiya zao na walitaka kufanya jambo ili kujaribu kuleta mabadiliko. Mifano kutoka katika muktadha wa nchi ya Marekani ni pamoja na Fight

For \$15 na Women's March. Mifano nyingine ambayo ina upeo wa kiulimwengu ni pamoja na Global Voices, Greenpeace na World Wildlife.

### **Ambia Wanafunzi Wako**

Sasa tunaenda kutambua jambo moja kwenye jamii yako unayofuatilia kwa dhati na hatua fulani ambazo wewe pamoja na jamii yako mnaweza kuchukua ili kutatua tatizo fulani.

## **Kazi**

## **Kazi**

### **Utoaji**

Wagawanye washiriki katika vikundi vya watu 3. Wape kila kikundi muda kwenye kikao cha sasa na angalau siku mbili kamili, ili 1) watafiti kuhusu tatizo linalokumba jamii yao, watambue angalau njia mbili ambazo tatizo hili linavyoathiri jamii yao na njia mbili zinazoweza kutumika kutatua tatizo hilo, na 2) kuunda bango lililo na maelezo kuhusu tatizo lililotambulishwa na suluhu zinazoweza kutumika ambazo watawasilisha kwenye kikundi kikubwa kama sehemu ya “gallery walk.”

### **Ambia Wanafunzi Wako**

Kwenye vikundi vyenu,

1. Fanya utafiti na utambue nyenzo ya jamuiya yako unayotaka kubadilisha (“jamii” inaweza kuwa shule, ujirani au kikundi chako cha mtaani). Unaweza kuongea na marafiki zako, walimu na/au familia kuhusu mambo ambayo wangependa kubadilisha au kuhusu matatizo yanayowakumba.
2. Unda bango. Bango lilioundwa na kila kikundi litatundikwa ukutani na tutafanya utalii wa “gallery walk” kwa pamoja ambapo kila kikundi kitajadili tatizo walilotambua na jinsi ya kulitatua.

Ni lazima kila kikundi kitambue angalau jinsi mbili tatizo hilo linavyoathiri jamii yao na njia mbili zinaweza kutumiwa kulitatua.

Kuwa mbunifu: piga picha na uzibandike kwenye bango ili kuonyesha tatizo na / au suluhu, au matumizi ya chati -tiririka, grafu na chati ili kuwasiliana kuhusiana na tatizo na/au suluhu [haswa, hakikisha kwamba washiriki wanaweza kufikia kichapishaji].

Kila bango linaweza “kujisimamia” – yaani, bango linapaswa kuwa na maelezo ya kutosha ili mtu aweze kuliona/kulisoma na kuelewa tatizo na suluhu zinazoweza kutumika bila mwanachama wa kikundi kueleza.

### **Utoaji**

Wape kila kikundi muda wa kutosha ili wajihusishe kwenye utafiti na kuunda mabango yao. Hakikisha kwamba upo kwa ajili ya kujibu maswali na kutoa usaidizi wa kiufundi. Wakati kikundi kikuu kinapojumuika pamoja tena, waarifu washiriki watundike mabango yao ukutani, kipe kikundi kikubwa zaidi dakika 20 ya kutembea na kuangalia mabango ya washiriki wengine, kisha utenge dakika 30 ili kila kikundi

kidogo kiwasilishe bango lake katika kikundi kikuu.